

## **HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 06/03/2022**

**KUHIDHINISHA FEDHA ZA UVIKO ZITUMIKE KWA FORCE ACCOUNT.**

### **AGENDA ZA KIKAO**

- 1.Kufungua kikao
- 2.Kuomba ridhaa ya matumizi ya FORCE ACCOUNT ya **Tshs.300,000,000.00**
- 3.Mengineyo.
- 4.Kufunga kikao.

### **WALIO HUDHURIA**

NAMBA	JINA	CHEO
01	Shija Lyella	Mwenyekiti
02	Omary Saidi	Katibu
03	Irine Mukerebe	Mjumbe
04	Nestori Mjojo	Mjumbe
05	Bruno Sangwa	Mjumbe

### **WASIOHUDHURIA**

NAMBA	JINA	CHEO	SABABU
01	Kelvini Lwegasira	Mwanasheria	Safari ya kikazi

### **GENDA NAMBA 1: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao cha bodi ya zabuni saa 3:00 alasiri kwa kuwakaribisha wajumbe wa bodi na kuwataka wawe watulivu.

### **AGENDA NAMBA 2 :KUOMBA RIDHAA YA MATUMIZI YA FORCE ACCOUNT TSH.300,000,000/=**

Mwenyekiti alimuomba katibu asome agenda namba mbili . Katibu wa bodi ya zabuni alisoma agenda namba mbili na wajumbe walianza kuijadili,Wajumbe waliomba aitwe mhandisi wa Halmashauri ili athibitishe kama anao wataalamu wa kutosha wa kuweza kusimamia mradi.

## **HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA**

Mhandisi wa halmashauri ndugu **Rajabu Mfinanga** alifika na kusema yeye anao wataalamu wa kutosha ambao wataweza kusimamia mradi huo na kukihakikishia kikao hakuna jambo litakalo haribika.

Baada ya kutoa maelezo hayo mwenyekiti alimruhusu Mhandisi aende na wajumbe waendelee kujadili,Mwenyeki aliwaruhusu wajumbe waendelee kujadili na ikiwezekana wakubali kwa Pamoja ili mradi uanze.

Wajumbe kwa Pamoja walikubali pesa hizo zitumiko kujenga jenga la dharula (EMD)kwa kutumia force akaunti lakini wakasisitisa taratibu ,sheria na kanuni za manunuzi zifuatwe ili kupunguza hoja za ukaguzi na kuleta ufanisi.

### **AGENDA NAMBA 3: MENGINEYO**

Mwenyekiti alimwambia Katibu asome ajenda inayofuata,Katibu alisoma ajenda namba tatu na kuwaacha wajume wachangie.

Wajumbe walimueleza Katibu wa bodi afanye kazi ya kuwaelimisha wajumbe wa kamati zitakazo undwa namna ya usimamizi wa mradi, na wakasisitiza kila kamati lazima awewe mwananchi mmoja au wawili kama muongozo wa force account uliotolewa na PPRA unayovyoelekeza .

### **KUFUNGA KIKAO:**

Mwenyekiti wa bodi alifunga kikao mnamo saa 3:30 alasiri na kumsisitiza Katibu awe makini kwenye mradi huu kwa kutafuta wazabuni wenyi sita ili waweze kuleta bidhaa kabla ya kulipwa fedha.

#### **Umedhibitishwa**

MWENYEKITI..... *shuja lyella*  
SAINI..... *Stella*  
TAREHE..... *12/03/2022*

KATIBU ..... *Omar Saini*  
SAINI..... *HDF*  
TAREHE..... *12/03/2022*